SOMO LA 25

KUSUDI LA MUNGU KWA WAYAHUDI

"Wao waliotawanyika, walisafiri hadi Foinike, Kupro na Antiokia wasilihubiri lile neno ILA KWA WAYAHUDI PEKEE YAO . " - Matendo 11:19

"Nimefungwa kwa mnyororo huu kwa ajili ya tumaini la Israeli." - Matendo 28:20

"Kwa maana ikiwa kutupwa kwao (Wayahudi) kumeleta upatanisho kwa ulimwengu, je! Kukubaliwa kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa?" - Rom 11:15

Wazo kwamba tumaini la injili linahusishwa na watu wa kisasa wa Kiyahudi na uanzishaji tena wa taifa la Israeli katika nchi ya Palestina ni la kigeni kabisa kwa mawazo ya Ukristo wa jadi. Hata hivyo, Biblia iko wazi kwamba uhusiano huo upo, na ni jukumu letu kuwa makini kutafuta maneno ya maandiko na kuelewa kwa nini jambo hili lipo na nini maana yake kwetu sisi.

Mvuto walio nao "Wakristo," kama kikundi, kwa Wayahudi, ni fikra za kijuujuu tu, na inahusiana zaidi na mambo ya kihistoria kuliko umuhimu wake wa siku za baadaye. Na inatokana na historia ya Wayahudi - kutoka kwa uhusiano wao wa kitaifa na Mungu katika nyakati za zamani, na kule kutumiwa na Mungu kama njia ya ufunuo wa Mungu; na kutokana na uhusiano wa mwili na damu yao na Masihi kwa kuwa Yesu mwenyewe alikuwa Myahudi. Hainyooshi picha ya siku zijazo, ila kwa hamu ya kiroho kwa Wayahudi, ambalo ni jambo la kibinadamu kwa ujumla. Haitambui kuwa wokovu wa watu inategemea moja kwa moja hali ya baadaye ya Wayahudi.

UJUMBE WA INJILI UNA VIZUIZI VYA KITAIFA!

Wokovu wa ulimwengu umefungamana na hatima ya Wayahudi. Katika somo hili tutajifunza kuwa bila utukufu halisi wa kitaifa wa Wayahudi, hakutakuwa na wokovu kwa watu binafsi au mataifa katika sura au muundo wowote. Mtu yeyote ambaye hajui au ana wasiwasi wa maendeleo haya ya baadaye kuhusiana na Wayahudi, anakosa sifa moja kubwa na muhimu ya mafundisho ya Biblia. Fikiria ushahidi huu. Yesu akawaambia wanafunzi wake –

"Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" - Mathayo 15:24

Hayo maneno "kondoo waliopotea ni dhahiri" yanamaanisha Wayahudi hasa > kutoka kauli nyingine kama hiyo ambayo haihusishi wote ila Wayahudi –

"Msiende kwa watu wa mataifa mengine, na katika mji wa Wasamaria msiingie; ila nendeni kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." - Mathayo 10:5,6

Yesu pia alimwambia mwanamke Msamaria, katika kisima cha Yakobo - "Wokovu watoka kwa Wayahudi" (Yohana 4:22).

Vifungu hivi vinaonyesha kuwa wokovu uliotangazwa na Yesu na mitume wake ulikuwa na mpaka wa kitaifa. Yesu alikuwa Myahudi, mzaliwa wa nyumba ya Daudi kama mrithi wa Mungu aliyeteuliwa kwa kiti cha enzi cha Daudi. Mitume ambao walifanya naye kazi pia walikuwa Wayahudi. Walitangaza ujumbe ambao ulikuja> kutoka kwa Mungu wa Wayahudi, na ambao kwa mujibu wa maelekezo ya awali ya Kristo ulikuwa na lengo tu la kuwafikia Wayahudi pekee. Kwa hivyo, Paulo angeweza kusisitiza kwa kuangalia injili kama "TUMAINI LA ISRAELI," hapo aliposema ...

" Nimefungwa kwa minyororo huu kwa ajili ya TUMAINI LA ISRAELI,." - Matendo 28:20. Pia alitoa kauli ifuatayo kwa msisitizo sana, katika kujitetea mwenyewe mbele ya mfalme Agripa ...

"Na sasa ninasimama hapa nihukumiwe kwa ajili ya tumaini la ahadi baba zetu waliyopewa na Mungu, ambayo kabila zetu kumi na mbili wanataraji kuifikia, wakimwabudu Mungu kwa bidii mchana na usiku, na MATUMAINI YA KUJA, NAMI NINASHITAKIWA NA WAYAHUDI KWA AJILI YA TUMAINI HILO, EE MFALME AGRIPA "- Matendo 26:6,7

Anaweza pia kusema kwa ukweli ambao ujumla haukubaliwi na wengi, "ndugu yangu, kwa jinsi ya mwili, ambao ni Waisraeli, wenye KUFANYWA WANA, na utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Mungu, NA AHADI "- Warumi 9:3-4. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba injili ya wokovu iliyotangazwa ili ikubaliwe ni ya Kiyahudi katika asili yake, matumizi yake, na kukua kwake kwa baadaye. Ni dhahiri pia kwamba hivi ndivyo ilivyochukuliwa na wanafunzi mara baada ya siku ya Pentekoste ...

"Wale waliotawanyika... Walisafiri hadi Foinike, Kupro na Antiokia wasilihubiri lile neno ila kwa Wayahudi pekee yao. " - Matendo 11:19.

MATAIFA HAWAKUITWA KWA INJILI HAPO AWALI

Petro alihitaji ufunuo maalum kumshawishi kuwa Mungu amewakubalia watu wa Mataifa kushiriki baraka za Israeli, na hata hivyo akamtupia Mungu wajibu huo. Hakujaribu kujihalalishia yeye mwenyewe, lakini akawaomba msamaha ndugu zake kwa kuwahubiria Watu wa Mataifa akisema,

"Mimi ni nani, niweze kumpinga Mungu?" - Matendo 11:17.

Ukweli ni kwamba, kukubaliwa au uandikishaji wa mataifa mengine kwa tumaini la Injili ulikuwa mojawapo wa "siri" ya injili iliyotajwa na Paulo, katika barua yake kwa Waefeso:

" Mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo, ambayo kwa vizazi vingine hawakujulishwa wanadamu kama walivyofunuliwa mitume na manabii wake watakatifu kwa njia ya Roho, ya kwamba watu wa mataifa ni WARITHI, na wa MWILI MMOJA, na

WANASHIRIKI pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. " - Waefeso 3:4-6.

Lakini ufunguzi wa njia kwa ajili ya uandikishaji wa Mataifa hakuwaharibia Waisraeli hali yao ya "MATUMAINI". Kwa kweli, athari hii ilikuwa vingine. Badala ya watu wa mataifa kubadili matumaini haya yawe ya Utaifa na mapokezi yao, matumaini yaliwabadilisha watu wa Mataifa, kuwa Wayahudi, zikaafikiana na tabia yake ya kimsingi ya Kiisraeli. Hivyo kauli ya Paulo kwa waumini wa Mataifa -

"Nyinyi mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ... Basi tangu sasa, ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu "- Waefeso 2:12.19.

"YEYE NI MYAHUDI kwa utu wa ndani "- Warumi 2:29.

... yaani, mtu yeyote ambaye si Myahudi kwa kuzaliwa, lakini ambaye anaelewa na anapokea tabia ya Wayahudi wa matumaini (yaani, kwamba ukombozi na wokovu inahusishwa na ahadi ambayo Mungu alimtolea Ibrahimu baba wa Wayahudi) ni Myahudi zaidi kuliko Yule halisi wa ukoo wa asili wa Ibrahimu asiyeelewa. Akizungumzia uandikishaji wa Mataifa, yeye anayeizungumzia kama kukata kutoka kwenye mzeituni, ambayo ni pori kwa asili, na kinyume kusanisha kwa asili, katika mzeituni ulio mwema (Warumi 11:24). Hivyo watu wa mataifa mengine ni "mzeituni yenye matawi pori," bila matumaini - bila haki ya kuzaliwa - bila ahadi - bila sehemu ya baadaye ya aina yoyote na kama wangeweza kuwa warithi wa urithi ujayo, ni lazima kutupiliwa mbali "mtu wa zamani" wa Utaifa wao, na kuvaa "utu mpya" wa Kiyahudi wa kweli ... "

... unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake aliyeuumba "- Wakolosai 3:10.

TUMAINI LA ISRAELI

Paul anasema kwamba alifungwa" kwa ajili ya tumaini la Israeli "(Matendo 28:20), ambayo ni sawa na kusema kwamba alihubiri" tumaini la Israeli " , kwa kuwa ilikuwa ni kwa mahubiri yake ndipo aliwekwa katika vifungo. Ni namna gani ndipo seti ya mawazo aliyohubiri Paulo kuitwa "tumaini la Israeli"? Ni kidogo sana kama kipo kinachofundishwa na Ukristo wa jadi ambacho kinaweza kusababisha kuitwa "tumaini la Israeli." Je, mahubiri ya Paulo yalitofautiana kivipi?

Kipengele muhimu cha mahubiri ya Paulo kilitambua Wayahudi kama tumaini la kitaifa, ukiwa na msingi juu ya ahadi fulani ambazo zilizotolewa na Mungu kwa akina baba wa taifa. Zile ahadi ambazo matumaini hayo yalitegemea, yako na "habari njema", au "injili" iliyotangazwa na Yesu na Mitume; na wale ambao waliamini walipata matumaini maalumu ya ukombozi na wokovu. Kutokana na hayo inakuwa wazi kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya matumaini ya Kikristo na tumaini la Israeli, kwa sababu wote wana msingi juu ya mapokezi ya mafundisho ya Injili. Ni lengo la somo hili kuchunguza muunganisho huo.

ASILI NA HISTORIA YA WAYAHUDI

Asili na historia ya Wayahudi imewekwa vizuri katika Biblia. Ibrahimu, mwanachama wa familia ya Babeli, aliamriwa kujitenga na watu wake, na kuingia katika nchi "ambayo anapaswa baadaye kupokea urithi" (Waebrania 11: 8). Alitii, akaenda huko, " asijue aendako." Aliarifiwa baadaye kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa, ambao Mungu atakuwa na uhusiano maalum nao, na ambao wanapaswa kuwa watu maalum wa utunzaji wake. Ikatokea nyumba ya Ibrahimu ilikwenda Misri, na kuketi katika nchi hiyo kama wakoloni walio na moyo wa kirafiki. Katika mfululizo wa matukio, Farao aliwafanya watumwa, na akawakabili na utawala wa uchungu kwa zaidi ya karne mbili. Mwisho wa wakati huo, walikombolewa kupitia kwa Mungu kwa mkono wa Musa; na baada ya kuzunguka kwingi na kupata ujuzi tosha, waliketi katika nchi ya ahadi kama ufalme ulio chini ya katiba ya Mungu, yaani, ufalme wa Mungu wa kwanza na wa awali duniani. Katiba hii ya Mungu iliwataka mradi wawe watiifu kwa mahitaji yake, wangebakia katika nchi hiyo kwa mafanikio makubwa, lakini mara tu watakapoondoka kwa msingi wa sheria za Mungu ambaye alikuwa amewaita na kuwafanya taifa, mashaka yangewapata. Sehemu inayofuata ya historia yao inajumulishwa katika kauli moja; walishindwa kutimiza hali ya agano la hilo taifa, wakagawanywa katika nchi mbili (Israeli na Yuda), na baada ya hapo walifukuzwa maeneo ya kitaifa kwa aibu, na kutawanyika miongoni mwa mataifa kama wakimbizi, ambako wamebakia kwa karne nyingi mpaka hivi majuzi walivyoweza kurudi tena kuwa taifa katika nchi ya Palestina. Mafundisho ya Kikristo ya Jadi haielezii zaidi ya muhtasari huu wa jumla wa historia ya Wayahudi. Kuwa Wayahudi wana aina yoyote maalum ya siku za baadaye katika mpango wa Mungu sio dhana inayovutia. Historia ya kitaifa ya wayahudi inaonekana kama yametimia, na hatima ya taifa imetiwa muhuri.

Mungu, hata hivyo, hufikiria kwa njia tofauti, na Biblia, neno lake pia, huongea tofauti. Fikiria ushahidi ufuatao kuhusu mahali pa taifa la Wayahudi mbele zake Mwenyezi Mungu: -

"Mimi Bwana ni mtakatifu nami nimewatenga ninyi na mataifa, ili kwamba mwe wangu" - Mambo ya Walawi 20:26

"Wewe u taifa takatifu kwa BWANA Mungu wako; BWANA Mungu wako, amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. "- Kumbukumbu la Torati 7:6

“Wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako, na Bwana amekuchagua kuwa watu wake hasa, kuliko mataifa yote yaliyo juu ya uso wa nchi"- Kumbukumbu la Torati 14:2

“Bwana amekuungama hivi leo kuwa WATU WAKE HASA, kama alivyokuahidi, na kuwa yakupasa kushika maagizo yake yote, na kuwa atakutukuza juu ya mataifa yote aliyoyafanya, kwa sifa, na kwa jina, na kwa heshima: nawe upate kuwa taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako "- Kumbukumbu la Torati 26:18-19

Itakuwa vigumu zaidi kutoa usemi wa mkazo kwa wazo hili maalum, makusudi, na lisilo na masharti kuhusu uteuzi na Mungu wa Wayahudi kama watu kwake. Sisi ni nani kusaili hilo? "Je!

Mfinyanzi hana amri juu ya udongo?" Mbona Muumba wa milele, katika hekima yake asiwe na haki ya kuwa na mipango yake mwenyewe kwa njia yake mwenyewe? Uteuzi wa Wayahudi ni sifa moja ya bwana aliye hodari wa kujipangia mambo kuhusiana na ulimwengu huu. Hii bila shaka limeonekana na ushahidi uliopo katika maandiko.

KWA NINI IWE NI MYAHUDI?

Biblia iko wazi kabisa kuwa uteuzi wa Myahudi kama taifa si kwa sababu ni Myahudi. Sio kwa sababu ya kustahili au kutokufaa kwao. Kama ingekuwa hivyo, wangekuwa wameangamizwa kitambo sana - sio tu kama taifa, lakini hata kama jamii. Uteuzi wa Myahudi, na kila kitu kinachotokea kwa Myahudi kinamhusu Mungu. Mungu amechagua kuwateua wao bila ya kujali hali yao ya maadili, KWA AJILI YAKE NA KWA UTUKUFU WAKE ...

"Sitendi hili kwa ajili yenu, Ee nyumba ya Israeli, bali KWA AJILI YA JINA LANGU TAKATIFU, mlilolitia unajisi katika mataifa mliyoyaendea. " - Ezekieli 36:22.

Hakuna kinachoweza kutengua uteuzi wa Mungu. "Zawadi na mwito wa Mungu hazina majuto (yaani mabadiliko). "Wayahudi wenyewe hawawezi kubatilisha amri hii. Huenda wakajiletea, kama wao walivyofanya, ghadhabu ya Mungu na mateso ya Mungu na dhambi zao, lakini hawawezi kubadilisha msimamo wao mbele ya Mungu kama taifa lake teule. Adhabu ambayo wao wamevumilia kwa vizazi vingi ni thibitisho maalum la Mungu kuwa nao. Lugha ya Mungu katika uhusiano wao ni maalum ...ama tuseme anawachukulia tofauti kabisa.

"Ni nyinyi tu niliowajua katika jamaa zote zilizo duniani, KWA SABABU HIYO nitawaadhibu maovu yenu yote." - Amosi 3: 2. Vivyo hivyo, majanga ambayo yaliwapata wao ni ushahidi wa usimamizi wa Mungu na kudhibiti kwake. Walitawanyika kwa sababu ya maovu yao, lakini sio kutupiliwa mbali daima, kama ilivyo wazo la kawaida: -

"Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua." - Warumi 11:2.

Ujumbe wa Mungu kupitia kwa Yeremia una uhakika zaidi ... "maana nitawakomesha kabisa mataifa yote huko nilikokutawanya, bali sitakukomesha wewe kabisa; lakini NITAKURUDI kwa hukumu, wala sitakuacha bila adhabu. " - Yeremia 30:11

Kuteseka kwa taifa la Israeli sio kingine bali ni marekebisho ya kipimo ambacho Mungu amewaingiza wao; lakini hakuna sehemu yoyote inaonyesha kuwa Mungu hatimaye amewakataa wao. Lugha ya kiroho ya Yeremia 33: 24-26 inaashiria kwamba baadhi, katika nyakati za zamani, walichukua mtazamo wa kinyume, na kugombana, kama wengi sasa wafanyavyo, kwamba Mungu alikuwa amewakana milele watu wake, na aliazimia uharibifu wao. Jibu lina mkazo na halina shaka ...

"Hufikiri neno hili walilolisema watu hawa, wakinena, jamaa zile mbili alizozichagua BWANA amezitupilia mbali. Hivyo ndivyo wanavyowadharau watu wangu, ili wasiwe taifa tena mbele yao. BWANA asema hivi, ikiwa agano langu la mchana na usiku halikai imara, na ikiwa mimi

sikuziamuru kawaida za mbingu na dunia, ndipo nitaitupilia mbali wazao wa Yakobo na Daudi mtumishi wangu. " - Yeremia 33: 24-26

KURUDISHWA KWA WAYAHUDI

Hivi sasa, Wayahudi wanateseka kutokana na ukaidi wao wa kiroho. Hii ilitabiriwa na manabii wote. Utabiri umenukuliwa vizuri. Ushahidi wa ukweli wao upo mbele ya macho yetu. Tunaiona ilivyoeenea katika utawanyiko wa taifa ambalo lilikuwa watu huru wa neno, Tunaiona iko katika hali hito ambayo wamekuwa wakifanyiwa na nchi zao zilizowalea (yaani Kuteketezwa).

Lakini haya yote yatabadilika: -

"BWANA asema hivi, kama nilivyoleta mabaya makuu haya yote juu ya watu hawa, vivyo hivyo nitaleta juu yao MEMA HAYO YOTE NILIYOWAAHIDIA. " - Yeremia 32:42.

Hapa pana jibu kamili kwa swali hilo. Uthibitisho wake ni kwamba mazuri yatashinda mabaya ambayo yamekuwa ni uzoefu wao. Hii ina maana kwamba wakati huu wa shida ya taifa utafikia mwisho. Angalia kwa makini, kuwa wema uliotabiriwa unatangazwa kuwa "ameahidiwa": Ni uzuri gani wameahaidiwa?

"Tazama, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapolitimiza NENO LILE NJEMA nililolinena katika nyumba ya Israeli, na katika habari za nyumba ya Yuda. Katika siku hizo, na wakati ule, nitamchipushia Daudi Chipukizi la Haki, naye atafanya hukumu na haki katika nchi hii. Katika siku zile Yuda ataokolewa, na Yerusalemu utakaa salama ".. - Yeremia 33:14,16

Hapa "jambo zuri liliahaidiwa" ni muhtasari wa kifupi. Sifa zake mbili kuu ni: (1) mfalme ili afanye hukumu na haki katika nchi na (2) ya wokovu wa Yuda na Yerusalemu katika siku yake. Hivi ni kama kusema ahadi ya Masihi kuwaokoa toka kwa maadui wao, na kuwapa afueni kutoka kwa dhuluma ambazo wamekuwa wakipitia kwa miaka mingi, ahadi ambayo inarejelewa mara kwa mara kwa maneno yafuatayo: -

"Nami nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo, juu ya milima ya Israeli na mfalme mmoja atakuwa mfalme wao wote, nao hawatakuwa tena mataifa mawili ". - Ezekieli 37:22

Zaidi ya hayo, ujumbe wa maandiko ni kwamba Wayahudi hawatarejeshwa tu, lakini wanafaa kuwaangamiza watu wa milki zote za dunia. Hata mataifa yenye nguvu kama Marekani na Uingereza, na kila uhisi wao wa kitaifa na kiburi, watafaa kujinyenyekeza au wapondwe na jiwe ambalo litafanywa jiwe kuu la pembeni –

"Wewe u rungu langu na silaha zangu za vita, kwa wewe nitawavunja-vunja mataifa; na kwa wewe nitaharibu falme ". - Yeremia 51:20

Ni muhimu kutambua kipengele cha pili katika jambo zuri lililoahidiwa: "Katika siku hizi Yuda ataokolewa, na Yerusalemu utakaa salama." Ni wazi siku hizi bado lakini zitakuja, kwa kuwa, kwa sasa hakuna Masihi anayetekeleza hukumu katika nchi ya ahadi, na hakuna makao salama

kwa Yuda na Yerusalemu, na kamwe mambo hayajawahi kuwa hivyo. Hata hivyo ahadi ni kwamba hili "jambo zuri" litakuja "kuwepo," hata baada ya taifa kuyapitia maovu haya yote ...

"Tena itakuwa, kwa kadiri nilivyowaangalia ili kung'oa, na kubomoa, na kuangusha, na kuangamiza, na kutesa, kwa kadiri iyo hiyo nitawaangalia, ili kujenga, na kupanda, asema BWANA. " - Yeremia 31:28.

Hii ni kwa kuwa katika siku ya "tawi la haki", yaani, siku za ufalme, wakati " atatawala na kufanikiwa, naye atafanya hukumu na haki katika nchi". Fikiria kauli ifuatayo:

"Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA, na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu; kwa ajili ya jina la BWANA, wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya. KATIKA SIKU HIZO, nyumba ya Yuda watakwenda pamoja na nyumba ya Israeli, nao watakuja pamoja, kutoka nchi ya kaskazini, mpaka nchi ile niliyowapa baba zenu iwe urithi wao. " - Yeremia 3:17,18

"Bwana MUNGU asema hivi, Tazama, nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda, nami nitawakusanya pande zote, NA KUWALETA KATIKA NCHI YAO WENYEWE." - Ezekieli 37:21

"Mimi nitachukua wewe toka kati ya mataifa, nami nitawakusanya na kuwatoa katika nchi zote, na KUWARUDISHA KATIKA NCHI YENU WENYEWE." - Ezekiel 36:24. Hakuna cha kukwepa lugha hii. Ni Dhahiri sana na huwezi kuichukulia au kuifafanua kishirikina au vibaya: -

"Lisikieni neno la Bwana, enyi mataifa, litangazeni visiwani mbali; mkaseme, Aliyemtawanya Israeli atamkusanya, na kumlinda, kama mchungaji alindavyo. kundi lake. " - Yeremia 31:10

Ikiwa ni kweli kwamba Wayahudi walitawanywa, basi watakusanywa tena. Kwa jambo hili ujumbe wa Biblia ni wazi; na wakati hili litakapotokea, Wayahudi wataheshimiwa sana sawa na vile wanavyodharauliwa kwa sasa ...

"Tazama, wakati huo ... nami nitamkusanya yeye aliyefukuzwa; nami nitawafanya kuwa sifa na jina miongoni mwa watu wote wa dunia, nitakapowarudisha wafungwa wenu mbele ya macho yenu, asema BWANA. " - Sefania 3: 19,20

"BWANA wa Majeshi asema hivi; Siku hizo watu kumi, wa lugha zote za mataifa, wataushika upindo wa nguo yake yeye aliye Myahudi, naam wataushika wakisema, Tutakwenda pamoja nanyi, kwa maana tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi. " - Zekaria 8:23

WAYAHUDI KUWA "TAIFA LA KWANZA" ULIMWENGUNI

Heshima hii inashikamana na ukuu wa kisiasa. Wayahudi watakuwa wenye nguvu zaidi na maarufu kati ya mataifa, na watu wote watakuwa chini ya mamlaka yao ...

"Mataifa wataijilia nuru yako, na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako... Na wageni watajenga kuta zako, na wafalme wao watakuwa wakiwahudumia;. Maana katika ghadhabu yangu nilikupiga, lakini katika upendeleo wangu nimekurehemu. Kwa hivyo, malango yako yatakuwa wazi daima; hayatafungwa mchana au usiku, ili watu wapate kukuletea utajiri wa mataifa mengine, ili wafalme wao waletwe. Kwa maana kila taifa na ufalme wa watu Wasiotaka kukutumikia WATAANGAMIA, ndio, MATAIFA HAYO WATAHARIBIWA KABISA. Wana wa watu wale waliokutesa, watakupigia magoti, na watu wote waliokudharau wewe watainama wenyewe chini ya nyayo za miguu yako; nao watakuita mji wa Bwana, Sayuni wa Mtakatifu wa Israeli. Na kwa kuwa umeachwa na kuchukiwa, hata ikawa. hapana mtu aliyepita ndani yako, Nitakufanya kuwa fahari ya milele , Furaha ya vizazi vingi "- Isaya 60: 3,10-12,14-15. Wakati haya yatatimizwa, maadui wa Israeli wataaibika. Wale ambao sasa wanawakejeli, na kuwafanyia mzaha juu ya matumaini yao ya kitaifa, watapatwa na adhabu ambayo wanajitafutia. Maadili yanayokaribia ya mafanikio ya Wayahudi yatakuwa kichocheo kwa uharibifu wao. Dalili za mwanzomwanzo za mabadiliko zitawajaza na hofu. Huu ni ujumbe wa maandiko yafuatayo ...

"Mataifa wataona, na kuzitahayarikia nguvu zao zote; wataweka mikono yao juu ya vinywa vyao;. Masikio yao yatakuwa na uziwi. Watayaramba mavumbi kama nyoka, watatoka katika mahali walimojificha, wakitetemeka; watakuja kwa BWANA, Mungu wetu, kwa hofu, nao wataogopa kwa sababu yako - Mika 7:16-17.

Hatima inayogofya itawapata ...

"Mimi nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana wako wokovu; na nitawalisha nyama yao wenyewe, nao watalewa kwa kuinywa damu yao wenyewe, kama kwa divai mpya na wote wenye mwili watajua ya kuwa mimi, BWANA, ni mwokozi wako, na mkombozi wako, ni Mwenye enzi wa Yakobo "- Isaya 49: 25-26.

“Tazama, wote walioona hasira juu yako watatahayarika na kufadhaika. Watu washindanao nawe watakuwa SI KITU,na KUANGAMIA. Utawatafuta wala hutawaona wale wapiganao nawe; watakuwa si kitu; watakuwa kama kitu kisichokuwa, wale waliofanya vita juu yako. "- Isaya 41: 11,12

Hapa, basi, ni baadhi ya adhabu kwa wote ambao sasa wanashirikiana dhidi ya Israeli, lakini kuna baraka iliyohifadhiwa kwa wale ambao ni marafiki wao. "Ana heri mtu akubarikiye, na alaaniwe kila akulaaniye." Hii ilikuwa amri iliyotamkwa kwa Balaamu chini ya ushawishi wa roho, na ilitangazwa kwa Ibrahimu karne zilizopita. Matumizi yake ni kwa mtu binafsi na taifa .

TAIFA LA WAYAHUDI LITASAFISHWA

Marejesho ya kitaifa kama kusudi la Mungu sio masharti juu ya marekebisho ya kitaifa.. Kwa hivyo kutakuwa na marejesho ya awali ya kitaifa yatakayosababisha maelfu ya Wayahudi waliokuwa wamekusanyika kutoka nchi ambako walitawanyika ambao kamwe hawataingia katika Nchi hiyo. Lakini hii haitaharibu uhusiano wao wa kitaifa. Wakiwa Wayahudi, ambao

Mungu amewachagua kama taifa maalum, kwa lengo la maendelezo ya kusudi lake kuu, kila mmoja wao atakusanyika katika marejesho ya awali .

"Naye atawatwekea mataifa bendera kwa mataifa, atawakutanisha watu wa Israeli waliotupwa, atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia" - Isaya 11:12.

Hata hivyo, ingawa watakusanywa kutoka nchi mbalimbali pasi ya kujali maadili, kujiunga na nchi itakuwa kwa msingi wa imani na maadili ya uadilifu wa kila mtu kibinafsi kwa taifa: - "Mimi nitawatoa katika mataifa, na kuwakusanya toka nchi mlizotawanyika ndani yake, kwa mkono hodari, na kwa mkono ulionyoshwa, na kwa ghadhabu iliyomwagika, nami nitawaingiza katika jangwa la mataifa, na huko ndiko nitakakoteta nanyi uso kwa uso. Kama nilivyoteta na baba zenu katika jangwa la Misri, ndivyo nitakavyoteta nanyi, asema Bwana MUNGU. Nami nitawapitisha chini ya fimbo, nami nitawaingiza katika mafungo ya agano, nami nitawasafisha kwa KUWATOA WAASI NA HAO WALIONIKOSA.Nitawatoa katika nchi wanayokaa ugenini, lakini hawataingia katika nchi ya Israeli. " - Ezekieli 20:34-38

Kwa jambo hili tunatambua usambamba wa tukio lile lilitokea baada ya wao kuondoka Misri chini ya Musa. Kisha walikuweko watu wasiofunzwa, watumwa wale wasioamini; na kizazi kizima, isipokuwa watu wawili - Kalebu na Yoshua - walikufa jangwani. Wao "hawakupata pumziko hilo kwa sababu hawakuamini," asema Paulo (Waebrania 4: 6). Kadhalika wengi wa Wayahudi wa kisasa wakati wa kurudi kwa Kristo pia watakuwa hawafai kuingia katika nchi; na Biblia inatwambia kwamba takaso sawa na hilo litafanyika jangwani, kama katika siku za Musa, na inaweza kuchukua kipindi kama hicho na / au kuwa na sura hiyo kwa ukamilifu wake: - " kwa mujibu wa siku ya kuja kwako kutoka katika nchi ya Misri nitamwonyesha kwa mambo yake ya ajabu. " - Mika 8:15

"Watu wako nao watakuwa WENYE HAKI WOTE waliotakaswa; nao watairithi nchi milele, tawi la upandaji wangu, kazi ya mikono yangu, ili mimi nitukuzwe" - Isaya 60: 21.

Hivyo , hata katika siku za marejesho ya taifa la Wayahudi, hali hiyo ya kukubaliwa na Mungu kwa Myahudi kutategemea masharti sawa na ya watu wa mataifa mengine; lakini matumaini ya watu wa mataifa yataegemea marejesho ya taifa la Wayahudi ambalo ni jambo muhimu sana kwa watu wa Mataifa. "Upofu kwa sehemu ilitokea kwa Israeli, MPAKA utimilifu wa Mataifa uwasili, na hivyo ISRAELI WOTE WATAOKOKA ... Ikiwa kosa lao limekuwa utajiri wa ulimwengu na upungufu wao umekuwa utajiri wa Mataifa, je! Si zaidi sana UTIMILIFU WAO? Ikiwa kutupwa kwao kumeleta upatanisho kwa ulimwengu, je! Kukubaliwa kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa? " - Warumi 11:25,26,28,12,15.

MASWALI KWA SOMO LA 25

1. Je, imani za kitamaduni na dhana ya Wakristo kwa ujumla hazitambui nini kuhusu mataifa ya Wayahudi?

2. Nini ilikuwa kizuizi cha ujumbe wa awali wa wokovu kitaifa iliyohubiriwa na Kristo na mitume?

3. Mojawapo ya "usiri" wa injili ilikuwa nini?

4. Kukubaliwa kwa watu wa Mataifa, katika matumaini ya Israeli kumeathiri vipi watu wa mataifa mengine?

5. Nini hufanya mtu kuwa Myahudi zaidi kuliko Myahudi halisi wa ukoo wa asili ya Ibrahimu?

6. Kuna uhusiano gani kati ya matumaini ya Kikristo na matumaini ya Israel?

7. Kwa nini Mungu amechagua taifa la Wayahudi kuwa watu wake wateule?

8. Majanga na adhabu kwa taifa la Wayahudi yamekuwa ni ushahidi wa nini?

9. Je, Mungu amekataa Wayahudi kama taifa lake teule?

10. Marejesho ya taifa la Wayahudi yatafanyika lini?

11. Je, Wayahudi wote wataingia nchi ya ahadi katika kipindi cha marejesho yao?

12. Je, kiwango tofauti kitatumika kwa wokovu wa Wayahudi tofauti na cha watu wa mataifa mengine?

13. Wokovu wa mataifa unategemea nini?